# Uchunguzi wa Nafasi ya Vijana katika Kudumisha Amani miongoni mwa Tamaduni za Waswahili katika mwambao wa Pwani ya Kenya na Tanzania

KUJENGA AMANI program
building peace together



©GETRUDEMALIZENI FOR WEWORLD

WeWorld Member of ChildFund Alliance
Peaceful Change initiative
HORN International Institute for Strategic Studies
University of Dar es Salaam
Co-funded by the European Union

Orodha ya Yaliyomo


3 **SHUKRANI**

**ORODHA YA VIFUPISHO**

4 **MUHTASARI**

6 **UTANGULIZI**

7 **MBINU YA UTAFITI**

**MATOKEO YA MSINGI**

8 Ni kwa namna gani vijana wanashiriki katika mijadala ya kijamii inayohusiana na amani, migogoro, na usalama

10 Mitazamo ya jamii juu ya vijana na jukumu lao katika masuala ya amani na usalama

10 Sababu zinazowakwamisha vijana kuwa na ushiriki chanya katika masuala muhimu ndani ya jamii zao

11 Udhihirishaji wa maadili, mila na desturi za utamaduni wa Waswahili

**UCHUNGUZI KIFANI KUTOKA TANZANIA**

13 Ni kwa namna gani vijana wanashiriki katika mijadala ya kijamii inayohusiana na amani, migogoro, na usalama

15 Mitazamo ya jamii juu ya vijana na jukumu lao katika masuala ya amani na usalama

16 Sababu zinazowakwamisha vijana kuwa na ushiriki chanya katika masuala muhimu ndani ya jamii zao

17 Udhihirishaji wa maadili, mila na desturi za utamaduni wa Waswahili

**UCHUNGUZI KIFANI KUTOKA KENYA**

19 Ni kwa namna gani vijana wanashiriki katika mijadala ya kijamii inayohusiana na amani, migogoro, na usalama

21 Mitazamo ya jamii juu ya vijana na jukumu lao katika masuala ya amani na usalama

21 Sababu zinazowakwamisha vijana kuwa na ushiriki chanya katika masuala muhimu ndani ya jamii zao

22 Udhihirishaji wa maadili, mila na desturi za utamaduni wa Waswahili

23 **HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

## Shukrani

Andiko hili limeandikwa na Anne Kristine Raunkiær-Jensen na Sophia Ngigi kutoka taasisi ya Peaceful Change Initiative chini ya mradi wa Kujenga Amani Pamoja unaotekelezwa na WeWorld na kufadhiliwa na Umoja wa Ulaya. Msingi wa andiko hili ni tafiti mbili zilizoandikwa na Dk. William John Walwa kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na timu ya utafiti kutoka Taasisi ya Kimataifa ya HORN ya Tafiti za Kimkakati (Horn International Institute for Strategic Studies), iliyoongozwa na Dk. Halkano Abdi Wario. Waandishi wangependa kuwashukuru watafiti tajwa na vyuo vikuu kwa kufanya utafiti wa awali, uchambuzi wa taarifa, na kuandaa ripoti za kina katika muktadha wa kila nchi. Aidha, washirika wa mradi katika kila eneo walikuwa na umuhimu katika kuwezesha ukusanyaji wa taarifa na kusaidia utafiti.

Kwa hiyo, waandishi wangependa pia kuwashukuru TABUFO (Mtwara), 4H (Tanga), Shirika la Vijana la Stretchers (SYO) na AZAKI na watafiti wengine wa ndani waliyofanikisha utafiti huu. Hatimaye, waandishi wangependa kumshukuru mtekelezaji mkuu wa mradi wa KAP WeWorld ambaye ametoa msaada wa kuongoza na kuratibu mchakato wa utafiti pamoja na Umoja wa Ulaya kwa kufadhili mpango huu.

*Chapisho hili limefadhiliwa na Umoja wa Ulaya. Yaliyomo ni wajibu pekee wa Peaceful Change Initiative, Taasisi ya Kimataifa ya HORN ya Tafiti za Kimkakati, na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na haiakisi maoni ya Umoja wa Ulaya.*

## Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| CBO | Asasi za Kijamii |
| AZAKI | Asasi za Kiraia |
| HL | Halmashauri za Wilaya |
| KAP | Kujenga Amani Pamoja |
| NGO | Mashiriki ya sio ya Kiserikali |
| INGO | Mashiriki ya Kimataifa ya sio ya Kiserikali |
| SACCO | Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo |
| VICOBA | Vikundi vya Akiba na Mikopo |

# Muhtasari

Andiko hili linajumuisha matokeo ya tafiti mbili zilizofanywa katika mwambao wa Pwani ya Waswahili nchini Kenya na Tanzania. Inachunguza uhusiano kati ya vijana, utamaduni na uimarishwaji wa amani na inataka kutambua nafasi muhimu za uongozi na ushawishi wa vijana wa kike na wa kiume katika kushughulikia masuala ya migogoro, usalama, na kuimarisha amani. Utafiti huu ulifanywa Kwale, Kenya na Taasisi ya Kimataifa ya HORN ya Tafiti za Kimkakati, kupitia watafiti wake, Dk Halkano Abdi Wario, Dk Hassan Khannenje na Daniel Iberi, na Tanga na Mtwara, Tanzania, na Chuo Kikuu cha Dar es Salam, kupitia mtafiti wake Dk William Walwa. Utafiti huu nchini Kenya na Tanzania ulifanyika kati ya Agosti na Septemba 2023 kupitia mahojiano maalum na majadiliano ya kikundi na wadau mbalimbali.

## MATOKEO YA UTAFITI

1

### Vijana hushiriki katika mijadala ya jamii kuhusu amani, migogoro, na usalama, hata hivyo, majukwaa mengi hujikita katika masuala ya usalama, huku yakiwatenga wanawake na hudhibitiwa na kutawaliwa na wazee.

Vijana hutumia majukwa yao wenyewe kuhamasisha amani, ikiwa ni pamoja na vyama vya Boda boda, asasi za vijana ngazi ya jamii (CBOs), na vikundi vya uwezeshaji wananchi kiuchumi (VICOBA). Sherehe za kitamaduni na kidini pia zinathaminiwa na jamii kama njia ya kuwaleta pamoja wanajamii, ikiwa ni pamoja na wale ambao hawausiki moja kwa moja katika mifumo rasmi ya usalama ngazi ya jamii. Hata hivyo, nyanja hizi mara nyingi hupuuzwa na hazitumiwi na wadau mbalimbali (kama vile Mashiriki ya sio ya Kiserikali, Mashiriki ya Kimataifa ya sio ya Kiserikali, na mamlaka za kitaifa na za mitaa) katika kuongeza ushiriki wa vijana katika masuala ya amani na utulivu.

2

### Mtazamo kwamba vijana hawawezi kuhamasisha masuala ya usalama na amani hukwamisha ushiriki wao katika masuala yanayohusu amani, migogoro, na usalama.

Vijana wa kiume kwa ujumla wanachukuliwa kama wahalifu wanaotuhumiwa kusababisha ukosefu wa usalama badala ya kuwa wadau wa amani, wakati vijana wa kike wakionekana kuwa na mchango duni katika nyanja za usimamizi wa usalama na masuala ya amani na migogoro. Hatakama mchango wa vijana ukitambuliwa, mara nyingi hujikita katika mifumo rasmi ya utawala au huwa chini ya uangalizi wa wazee.

3

### Sababu zinazowakwamisha vijana kuwa na ushiriki chanya katika jamii hutofautiana kati ya muktadha, hata hivyo, kikwazo kikuu huwa ni tabia ya wazee kiume kuhodhi maamuzi katika majukwa ya kiraia.

Hii ni pamoja na kuminywa kwa fursa za vijana kupata rasilimali za kiuchumi, kama vile ardhi. Uwepo wa mfumo dume humaanisha kuwa vijana wa kike wanakabiliwa na vikwazo vya ziada. Kuna kutokuaminiana baina vijana na wazee, na hasa kati ya vijana na wadau mbalimbali wa masuala ya usalama. Licha ya hayo yote, vijana wana mchango mkubwa katika juhudi za kudumisha amani na usalama.

4

### Mila, desturi na maadili ni vyanzo muhimu vya mshikamano wa kijamii, na fursa muhimu ya kuimarisha ushirikishwaji wa vijana, na hasa vijana wa kike.

Msingi wa maadili, mshikamano na ukarimu miongoni mwa wanajamii huwaleta watu pamoja na hukuza umoja ndani na nje ya nchi. Sherehe za kidini na kimila ni majukwa muhimu yasio rasmi ambayo hutumika kujadili masuala ya amani na usalama. Hata hivyo, kadri muda unavyokwenda desturi hii inapotea, hususani nchini Kenya, na kwa sasa desturi hii imebaki kuwa ni ya wazee.

## MAPENDEKEZO

Mapendekezo ya utafiti huu ni pamoja na umuhimu wa kutambua na kuthamini mila na desturi kama nyanja muhimu katika kudumisha amani 'kila wakati'.

Jitihada madhubuti zinahitajika ili kubadilisha mitazamo ya vijana na kuimarisha uhusiano kati ya vijana na wazee, kwa mfano kupitia mazungumzo baina yao ambayo yataleta tija katika kuongeza mchango wa vijana katika kudumisha amani na utulivu. Jitihada mahususi zinahitaji ili kuimarishwa hali ya kuaminiana baina ya vijana na mamlaka, hasa vyombo vya usalama, kupitia mbinu ambayo inasaidia mamlaka hizi kuona thamani ya mchango wa vijana kwenye kazi zao. Kadhalika uimarishaji wa asasi za vijana kungewawezesha kuziwajibisha mamlaka za mitaa na kuchagiza ushirikishwaji wa vijana wa kiume na wa kike katika nafasi za maamuzi. Hususani, ushirikishawaji wa vijana hasa vijana wa kike ambao walikuwa wametengwa katika maamuzi yanayohusu masuala ya amani na usalama katika jamii.

# Utangulizi

Vijana wa kiume na wa kike kote katika Pwani ya Waswahili wana umuhimu mkubwa katika juhudi za kujenga na kudumisha amani katika jamii zao, lakini mara nyingi wanatazamwa kama watuhumiwa wanaosababisha migogoro badala ya kutazamwa kama wadau muhimu wa kiumarisha and kudumisha amani. Kuna uelewa finyu kuhusu mchango wa utamaduni wa Waswahili katika kuhamasisha ushiriki wa vijana katika masuala ya amani, migogoro, na usalama. Vivyo hivyo, kuna uelewa duni kuhusu mchango wa tamaduni za Waswahili katika kuhamasisha umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii katika Mwambao Pwani ya Afrika Mashariki.

Kwa kuzingatia utafiti uliyofanywa katika jamii za ukanda wa pwani ya Waswahili hasa maeneo ya Kwale nchini Kenya, na Tanga na Mtwara nchini Tanzania, chini ya mradi wa Kujenga Amani Pamoja (building the peace together), andiko hili linachunguza uhusiano kati ya vijana, utamaduni, na ujenzi amani.[1] Utafiti huu unalenga hasa kubaini majukwa muhimu yaliyopo ambayo yatawezesha vijana wa kike na kiume kushiriki na kushawishi maamuzi muhimu yanayolenga kushughulikia masuala ya migogoro, usalama, na uimarishwaji wa amani, pamoja kuibua namna mila na desturi zinavyoweza kutumika katika kuhamasisha mshikamano, majadiliano, na ushirikiano wa jamii. Hata hivyo, kuna haja ya kuchukua tahadhari juu ya baadhi ya mila na desturi katika utamaduni wa Waswahili ambazo hazihamasishi au zinalenga kuendeleza ukandamizaji wa kitabka kama vile ukandamizaji wa kijinsia. Utafiti huu unalenga kubainisha nyanja na mila na desturi chanya ambazo hupatikani katika jamii za ukanda wa pwani.

Andiko hili limeandaliwa na Peaceful Change initiative (PCi) na limejikita katika tafiti mahususi kutoka Kenya na Tanzania ambapo linawasilisha matokeo ya utafiti kwa muktadha wa Kenya na Tanzania huku likijumuisha matokeo ya msingi ya utafiti na mapendekezo kutoka nchi tajwa.

## Kujenga Amani Pamoja

Mradi wa Kujenga Amani Pamoja ni mradi wa miaka mitatu unaotekelezwa na WeWorld kwa msaada wa Peaceful Change initiative (PCi), Tanzania Building Future Organization (TABUFO), 4H, Stretchers Youth Organisation (SYO), na Conselho Nacional de Voluntariado (CNV) kutoka 2023 hadi 2026 na kufadhiliwa na Umoja wa Ulaya.Mradi huo unalenga ukanda wa pwani hasa katika kaunti ya Kwale (kwenye tarafa za Msambweni, LungaLunga, na Matuga) nchini Kenya, mkoa wa Tanga (kwenye halmashauri za Mkinga na Pangani) na mkoa wa Mtwara (kwenye halmashauri za Mtwara, Tandahimba, na Newala) nchini Tanzania, na jimbo la Cabo Delgado (kwenye wilaya za Ancuabe, Chiure, na Mecufi) na jimbo la Nampula (kwenye wilaya ya Erati) nchini Msumbiji.

Mradi huu unatarajia kuendeleza mila na desturi chanya za tamaduni za Waswahili katika kuwasaidia na kuwawezesha vijana kuimarisha na kudumisha amani ndani ya jamii zao.

*

## Utamaduni wa Waswahili

Kwa kutambua historia pana na tata ya jamii na tamaduni za watu wa pwani, utafiti huu unaelezea dhana ya Utamaduni wa Waswahili kuakisi mila na desturi mbalimbali za jamii za watu wa mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki ambao ndiyo walengwa wakuu wa utafiti huu.

1. Utafiti wa tatu mahususi, unaangazia Kaskazini mwa Msumbiji, kwa sasa unaendelea na umepangwa kuchapishwa mnamo mwaka 2024.

# Mbinu (Methodolojia) ya Utafiti

Utafaiti huu ulifanyika Tanzania na Kenya kwa kutumia mbinu ya kitaamuli(shirikishi) ikiwa ni pamoja na kurejelea makala mabalimbali, mahojiano na majadiliano mahususi na wadau wa jamii katika maeneo yaliyochaguliwa. Washiriki  wa utafiti walichagiliwa kwa kuzingatia uwakilishi sawia kutoka katika  maeneo yao, usawa wa kijinsia, pamoja na uwakilishi sawia kutoka kwa makundi  ya umri, na asili ya kikabila ili kutoa mtazamo wa kina kuhusu mienendo ya jamii inayohusiana na mahusiano na miingiliano iliyopo baina ya vijana, utamaduni na amani. Vivyo hivyo , utafiti ulilenga kukutana na kufanya mashauri  na mamlaka na wawakilishi wa serikali wanaohusika na masuala ya utamadani na usalama,  viongozi wa jumuiya zisizo rasmi, vijana ambao wanashiriki  katika shughuli za kiraia na wale ambao hawashirika.

Utafiti huu ulikabiliwa na changamoto kadhaa, kubwa ikiwa ni wakati wa uchunguzi wa nafasi na mchango chanya wa vijana wa kike katika masuala ya amani, migogoro, na usalama. Mara nyingi washiriki wa kike walirejelea mifano ya ushawishi na michango ya vijana wa kiume badala ya vijana wa kike. kwa kiasi fulani suala hili linachangiwa na kanuni na mtazamo wa majukumu ya kijinsia ambapo masuala yanayohusiana na amani, migogoro na usalama hutawaliwa na wanaume na kutambulika kama eneo la wanaume ambalo wanawake hawana umuhimu. Kwa kuzingatia utafiti huu, jitihada zaidi zinahitajika katika kuchunguza na kuhamasisha mchango na nafasi ya vijana wa kike katika masuala ya amani, migogoro na usalama. Zaidi ya hayo, ingawa utafiti wa awali ulionyesha kuwa utamaduni wa Waswahili unahamasisha umoja na mshikamano katika kijamii, matokeo ya utafiti huu  yanaonesha kuwa utamaduni wa waswahili una mapungufu katika masuala ya usawa wa kijinsia. Hivyo basi, Utafiti wa kina unahitajika zaidi katika masuala ya kijinsia kama ripoti hii inavyoainisha ili kutanabaisha mikakati ya ushiriki kwa makundi yote katika jamii.

Ingawa tafiti hutumia zana na mbinu za ukukusanyaji wa data zinazofanana, matokeo yake huwa yanaakisi upekee wa muktadha mahususi. Hivyo, katika utafiti huu matokea yake yanafanana kwa kiasi kikubwa kati ya muktadha na utofauti ni wa kiwango cha chini.



# Matokeo ya Msingi

## 1 Namna vijana wanavyoshiriki katika majadiliano ya jamii kuhusu amani, migogoro, na usalama

Vijana katika ukanda wa Pwani ya Waswahili (maeneo ya Kwale, nchini Kenya na Tanga na Mtwara, nchini Tanzania) hushiriki katika mijadala ya jamii inayohusu masuala amani, migogoro, na amani kupitia majukwaa mbalimbali rasmi na yasio rasmi.

Serikali, polisi na vyombo vingine vya usalama hupendelea zaidi matumizi ya mifumo rasmi ya Polisi Jamii kama vile ulinzi shirikishi, sungusungu na mgambo (Tanzania), Nyumba kumi (Tanzania na Kenya) , na kamati za amani (Kenya). Ingawa utafiti ulionyesha kuwa mifumo kama hii imeonyesha ufanisi kwa kiasi fulani katika kuwashirikisha vijana katika kudumisha usalama katika jamii zao. Mifumo hii huwa inatekelezwa kwa kuanzia ngazi ya juu kushuka chini, pamoja na kujitenga na utamaduni wa jamii husika na bila uwepo wa vijana katika nafasi za uongozi, pia inatawaliwa na wanaume na inakosa uendelevu na ustahimilivu wa kifedha.

Ingawa mifumo rasmi ya usalama kama hii inajumuisha nafasi muhimu ambamo ushiriki wa vijana unapaswa kuimarishwa. Utafiti huu umefichua kuwa kuna majukwaa mengine ambayo viwango vyake vya urasmi vinatovyautiana lakini yana umuhimu mkubwa katika kukuza ushiriki na ushawishi wa vijana. Hata hivyo, majukwaa hayo hayathaminiwi na kutumiwa ipasavyo na mamlaka zilizopo. Majukwaa hayo ni  kama vile  sherehe za kimila na kidini, maeneo ya mikusanyiko isio rasmi kama vile Maskani, Vijiwe'[2] , Vyama vy waendesha boda boda,  asasi za vijana ngazi ya jamii na vikundi vya uwezeshaji wanawake kiuchumi (VICOBA).

Jamii nyingi za Waswahili katika mwambao wa Afrika Mashariki huthamini sana sherehe za kimila na kidini, mathalan harusi na mazishi, na ngoma na nyimbo za asili. Sherehe hizo zimekita mizizi katika tamaduni za jamii husika na huwaleta pamoja watu mbali mbali ndani na nje ya jamii husika ili kushirikiana, hasa wakiwemo wale ambao hawausiki moja kwa moja katika mifumo rasmi ya usalama ngazi ya jamii. Hata hivyo, mamlaka zinauelewa finyu kuhusu tija na umuhimu wa mifumo tajwa ya kitamaduni ngazi ya jamii na huidharau kwa kuhitimisha kuwa ni nyanja za burudani ambazo huchochea umasikini na uvivu katika jamii.

Taasisi za dini kwa ujumla hutukuzwa sana ndani ya jamii na mara nyingi huwa zina mchango chanya katika utatuzi wa migogoro na ushirikishwaji wa vijana, katika baadhi muktadha huwa ni kiunganishi kati ya vijana na mamlaka na wadau mbali mbali wa usalama. Hata hivyo, jitihada zinahitajika ili kuimarisha nafasi za ushirikishwaji na uongozi wa vijana na wanawake ndani ya taasisi za dini.

**Jamii nyingi za Waswahili katika mwambao wa Afrika Mashariki huthamini sana sherehe za kimila na kidini, mathalan harusi na mazishi, na ngoma na nyimbo za asili.**

2. Maskani ni neno linalotumiwa nchini Kenya kurejelea maeneo ambapo vijana hukutana, kukaa na kuzungumza mara kwa mara baada ya kazi kwa ajili ya burudani na kubadilishana mawazo. Vijiwe inarejelea maeneo yanayofanana lakini ni neno linalotumika nchini Tanzania.




Ulinzi shirikishi ni utaratibu wa Polisi Jamii ambao unajumuisha vikundi vya vijana wa kiume vilivyoratibiwa na serikali ya mtaa ambapo vijana huungana kwa pamoja na kushiriki katika vitengo vya doria vilivyopewa mamlaka ya kusimamia ulinzi na usalama katika vitongojivyao. Sungusungu ni mfumo wa Polisi Jamii ambao uliundwa na kupitishwa kwa lengo la kulinda na kudumisha ulinzi na usalama katika maeneo yenye viashiria vya ukosefu wa usalama, hasa maeneo ya mpakani. Mfumo wa Sungusungu hutekelezwa na wanajamii wa kiume kwa kufanya doria nyakati nyakati za usiku na wakati mwingine mchana ambapo hali ya ukosefu wa usalama ni kubwa. Mgambo (Jeshi la Akiba) inajumuisha wanajamii waliopata mafunzo ya msingi au awali ya kijeshi na husaidia serikali za mitaa katika masuala ya usalama.Nyumba kumi (Ubalozi) ni mfumo wa Polisi Jamii ambapo wakazi wake hupangwa katika makundi ya kaya kumi, na kila ubalozi una kiongozi wake (balozi). Viongozi hawa wana wajibu wa kuwasiliana na polisi na vyombo vingine vya usalama, pamoja na kuwafahamisha wanajamii wao kuhusu vitisho vya usalama na masuala mengine ya jamii kwa Polisi.

Umuhimu wa vyama vya madereva wa boda bado (teksi za pikipiki) unazidi kukua ndani ya jamii, hususani katika masuala ya kudumisha amani na mshikamano katika jamii. Hata hivyo, mamlaka zina mtazamo hasi juu yao ambamo wanawachukulia kama wahalifu wanaosababisha ukosefu wa amani, na hii ni kutokana na uhusiano mbovu uliopo baina yao. Ushirikiano wenye tija na sekta ya bodabaoda ni hatua muhimu katika ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya amani na usalama

Nchini Kenya (hasa Kwale), Asasi za Kiraia (AZAKI), Mashirika yasio ya Kiserikali (NGOs) na Asasi za kijamii (CBOs)) ni majukwaa makuu ya ushirikishwaji wa vijana na uongozi katika masuala ya usalama, migogoro na amani ambayo hushirikiana na maeneo mengine kama vile waendesha boda boda na sherehe za kijamii kama vile harusi. Ingawa nchini Tanzania, jukumu la asasi za kiraia halikuonekana katika utafiti, pengine nafasi na uwezo wa asasi za kiraia nchini Tanzania kwa ujumla ni finyu ikilinganishwa na Kenya. Ijapokuwa asasi za kiraia zina uwezo finyu wa kuwafikia na kuwashirikishi vijana wengi, bado yanayo nafasi ya kutoa utaratibu muhimu wa ushiriki wa vijana na hasa kwa ushirikishwaji na uongozi wa wanawake ambao wanajikuta wametengwa kutoka kwenye majukwaa mengine yanayoshuhulikia masuala ya usalama.

Kwa ujumla, majukwaa mengi katika ukanda wa Pwani ya Waswahili huthibitiwa na kutawaliwa na wazee na wanaume. Hivyo, hali hii husababisha ukosefu wa ushirikishwaji wa vijana na wanawake. Jitihada mahususi zinahitajika miongoni mwa mamlaka, vijana, wanawake, na wazee katika kukuza wigo wa ushirikishwaji wa vijana wa kike na kiume katika majukwaa mbalimbali na uongozi.

## 2 Mitazamo ya jamii juu ya vijana na jukumu lao katika masuala ya amani na usalama

Mchango wa vijana wa kiume na wa kike katika Ukanda wa Pwani ya Waswahili (Afrika mashariki ) katika masuala ya amani na usalama unakwamishwa na mitazamo potofu kuwa vijana hawana uwezo thabiti wa kuongoza na kuhamasisha masuala ya amani na usalama. Vijana wa kiume kwa ujumla wanachukuliwa kama wahalifu wanaotuhumiwa kusababisha ukosefu wa usalama badala ya kuwa wadau wa amani, wakati vijana wa kike wakionekana kuwa na mchango duni katika nyanja za usimamizi wa usalama na masuala ya amani na migogoro kutokana na mitazamo mbalimbali ya majukumu ya kijinsia.

Mifumo rasmi ya kimamlaka na wazee hutambua kwa kiasi fulani majukumu ya vijana katika masuala ya amani na usalama; hata hivyo, hujikita katika mifumo rasmi ya utawala au huwa chini ya uangalizi wa wazee. Mitazamo hii hasi juu ya vijana inahitaji kushughulikiwa na kubadilishwa ili kuweka mazingira mazuri kwa vijana wa kiume na wa kike kushiriki ipasavyo katika masuala ya jamii kuhusu amani na usalama.

## 3 Sababu zinazowakwamisha vijana kuwa na ushiriki chanya katika jamii

Mbali na mitazamo hasi na potofu ya jamii juu ya vijana katika ukanda wa Pwani ya Waswahili, Kuna sababu nyingine nyingi zinazowakwamisha vijana katika kutoa mchango chanya ndani ya jamii. Nchini Tanzania, utafiti umebainisha kuwa Vijana wanakabiliwa na changamoto kuu mbalimbali ambazo ni kubaguliwa na kutengwa, matatizo ya kiuchumi na uwepo wa dini zenye itikadi na misimamo mikali, na nchini Kenya changamoto za uendeshaji wa asasi za kiraia zilibainishwa na kusisitizwa. Licha ya juhudi mahususi za AZAKI zinazoongozwa na vijana katika kijiji cha Kwale, wazee hawana imani nazo na wanaziona kuwa sio endelevu na stahimilivu.

Vijana wanakabiliwa na changamoto ya kutengwa katika kufanya maamuzi ambayo yanadhibitiwa na kutawaliwa na mamlaka na wazee, hasa wazee wa kiume, na ukosefu wa rasilimali za kiuchumi (kama vile ardhi). Sababu hizi zinadidimiza uwezo wa vijana wa kuwa na mchango chanya ndani ya jamii. Haya yote, yanachagizwa na uwepo wa mfumo dume ambao hutanabaisha na kufafanua majukumu ya kijinsia, ambapo vijana wa kike hukabiliwa na vikwazo vya ziada vya kutengwa.

Uhusiano kati ya vijana na watendaji wa usalama (hasa kati ya boda boda na polisi) ni mbovu na umetawaliwa na kutokuaminiana. Zaidi ya hayo, uwepo wa itikadi kali za kidini huchangia zaidi kutengwa kwa vijana kutoka kwa jamii yote na huweka vikwazo katika shughuli za kijamii zinazohamasisha mshikamano wa kijami.[3]

Huko Kwale, nchini Kenya, ambako asasi za kiraia ni jukwaa la msingi katika ushiriki wa vijana katika masuala amani na usalama, changamoto kuu zilizoangaziwa na kubainishwa ni pamoja na uhaba wa rasilimali fedha, ukosefu wa ujuzi katika uendeshaji wa mashirika, ukosefu wa msaada kutoka kwa mamlaka na wanajamii kwa ujumla, na uwakilishi usio ridhisha wa vijana wa kike.[4]

3. Ingawa masuala haya hayakubainishwa katika utafiti uliofanyika nchini Kenya, uchambuzi wetu wa migogoro unapendekeza kuwa ni sababu za msingi zinazochochea migogoro huko Kwale na kuwa na athari hasi kwa vijani.
4. Asasi za kiraia nchini Tanzania zinakabiliwa na vikwazo vya ziada vya nafasi na uwezo ambao unahitajika katika kushughulikia na kuimarisha jukumu lao kama wadau muhimu katika ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya amani.

## 4 Udhihirishaji wa maadili, mila na desturi za utamaduni wa Waswahili

Maadili, mila na desturi zinazoshikiliwa na jamii za Pwani ya Waswahili huko Kwale, nchini Kenya, na Tanga na Mtwara,nchini Tanzania ni vyanzo vya msingi vya mshikamano wa kijamii. Utamaduni wa jamii za Pwani ya Waswahili umefungamana sana na dini.

Utafiti huu umetoa mwanga na ufahamu kuhusu namna maadili ya ukarimu na kujaliana (dhana hizi hutumika kuelezea kuwa watu wote ni ndugu) yanavyowaleta watu pamoja na kukuza ushirikiano wa kijamii na hivyo kuchangia mshikamano wa kijamii ndani na hata nje ya jamii.

Mikusanyiko ya sherehe za kidini na kimila huimarisha uhusiano wa wanajamii wanaoishi ndani na nje ya jamii, ambapo wanafamilia hurudi makwao wakati wa sherehe. Pia hutumika kama majukwaa ya kubadilishana mawazo na majadiliano kuhusu masuala ya amani, migogoro, na usalama.

Nchini Tanzania, ngoma za kitamaduni (kimila) na muziki zilibainishwa kuwa nyenzo muhimu katika kukuza na kusambaza jumbe za amani na hutumika kama majukwaa ya usuluhishi na upatanishi katika jamii.

Huko Kwale, Nchini Kenya, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa mila na desturi za kitamaduni hazijaenea sana katika jamii ya leo. Hii inathibitishwa na data zilizokusanywa ambapo, uchambuzi umebainisha kuwa mila na desturi za kizazi cha zamani hazijachukuliwa na kizazi kipya. Hata hivyo, utafiti ulibainisha kuwa mila na desturi za utamaduni huhimiza amani na ushirikiano katika jamii. Mila na desturi za vizazi vya nyuma zinaweza kuchukuliwa na kutumiwa kama nyanja ya muhimu kataika ushirikishwaji wa vijana.




©PHOTOVOICE WEWORLD

**Maadili ya ukarimu na kujaliana huwaleta watu pamoja na kukuza mshikamano wa kijamii na hivyo kuchangia utengamano wa kijamii ndani na hata nje ya jamii.**

## Uchunguzi Kifani Kutoka Tanzania

Uchunguzi kifani huu unachunguza nafasi ya vijana katika kujenga amani na uwezekano wa kutumia utamaduni wa Waswahili katika kuhamasisha na kudumisha amani katika mikoa ya Mtwara (kwenye wilaya za Tandahimba, Newala na Mtwara) na Tanga (katika wilaya za Mkinga na Pangani) nchini Tanzania.



## 1 Ni kwa namna gani vijana wanashiriki katika mijadala ya kijamii inayohusiana na masuala ya amani, migogoro, na usalama

Utafiti uliibua majukwaa mbalimbali ambayo vijana hushiriki katika mijadala ya kijamii kuhusu masuala ya amani, migogoro, na usalama. Majukwaa hayo yanaratibiwa kupitia utaratibu wa Polisi Jami kama vile ulinzi shirikishi, sherehe na desturi za kitamaduni, vyama vya waendesha Boda Boda, mikusanyiko isio rasmi ya kidini na kijamii.

Utafiti ulibainisha mifumo mbalimbali ya Polisi Jamii (ikiwa ni pamoja na sungusungu, mgambo, na nyumba kumi). Hata hivyo, ilibainika kuwa mfumo wa ulinzi shirikishi uliopo kwenye muundo wa serikali china ya mpango wa Polisi Jamii ndio mfumo unaongoza kwa kuwamasisha vijana katika harakati na majadiliano yanahusu masuala ya amani, migogoro, na usalama. Ulinzi shirikishi inaungwa mkono sana na serikali na polisi na umeonyesha ufanisi katika kuwashirikisha vijana kwenye jamii katika kusaidia kupunguza vitishio vya usalama hususani katika wilaya za mpakani za Tanga na Mtwara.

Hata hivyo, utafiti uliibua changamoto kadhaa zinazoukabili mfumo wa ulinzi shirikishi kama njia ya madhubuti ya ushirikishwaji wa vijana katika masuala ya amani, migogoro, na usalama. Kwanza, ulinzi shirikishi sio jumuishi; hutawaliwa na wanaume na hutambulika kama eneo la wanaume ambalo wanawake hawana umuhimu. Pili, muundo na uendeshaji wa  ulinzi shirikishi huanzia ngazi ya juu kushuka ngazi chini na kufanya ujitenge na jamii na utamaduni wake. Vijana wanaoshiriki katika vitengo vya doria huhamasishwa na viongozi na maafisa wa serikali za mitaa na polisi, na vitengo hivi vya doria hutoa ripoti kwa polisi na serikali za mitaa na sio kwa  jamii. Mwisho, mfumo wa ulinzi wa shirikishi sio endelevu na stahimilivu kiutendaji wala kifedha; unafanya kazi kama gari la wagonjwa, unafanya kazi wakati vitisho vya usalama vinapoongezeka na kutoweka vinapopungua. Washiriki hawafidiwa kifedha bali wanategemea michango kutoka kwa wanajamii ambayo ni adimu katika wilaya za vijijini kama Mkinga, Pangani, Tandahimba na Newala ambako wanajamii hawana uwezo wa kulipa. Kutokana na hali hiyo, baadhi ya vijana hukataa kushiriki katika masuala ya ulinzi shirikishi, kwani ushiriki wa muda mrefu katika vitengo vya doria huingilia shughuli zao zinazowazalishia kipato. Katika baadhi ya matukio, hii imezua mvutano kati ya wale walioendelea kushiriki na wale ambao waliacha, huku wa kwanza wakiwashutumu wa pili kuwa ni wafuasi na washirika wa ghasia za itikadi kali.

Kwa upande wao, wanajamii na vijana walielezea kuwa ngoma na muziki wa asili ni nyanja mathubuti na inayopendelewa hivyo huleta umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii. Sherehe za kimila na kidini (kama vile harusi, sikukuku za Maulid) ) zinaendelea kuvutia ushiriki wa vijana wa kiume na wa kike katika masuala ya jamii yao, ikiwa ni pamoja na masuala ya amani na usalama. Maadhimisho haya pia yanaunganisha wanajamii katika ndani na nje mipaka ya taifa, yaani wanajamii wa kabila la Digo katika Wilaya ya Mkinga, Tanga na Kaunti za Kwale na Mombasa nchini Kenya, na wanajamii wa kabila la Makonde huko Mtwara, Tandahimba na Kaskazini mwa Msumbiji.[5]

5. Kudorora kwa usalama kwenye mpaka wa Mtwarana Kaskazini mwa Msumbiji kumedhoofisha uwezekano wa ushirikiano wa jamii na vijana kupitia maeneo ya kitamaduni huku serikali ikiweka vikwazo kwa mikusanyiko ya kitamaduni ili kukabiliana na mashambulizi yanayofanywa na kundi lenye ghasia za itikadi kali linalojulikana kwa jina la Al-Shabbab.

Hata hivyo, maafisa wa serikali na polisi walionyesha uelewa finyu kuhusu tija na umuhimu wa mifumo ya utamaduni katika kuhamasisha ushiriki wa vijana katika masuala ya amani,migogoro,na usalama. Wana mitazamo hasi, juu mifumo ya kitamaduni na huhitimisha k wa kusema kuwa muziki na ngoma za asili, matambiko, mikusanyiko isiyo rasmi na sherehe za sherehe za kitamaduni huchochea uvivu na ni chanzo na sababu ya umaskini.

Umuhimu wa vyama vya madereva wa bodaboda katika kuhamasisha ushiriki wa viajana katika majadiliano yanayohusu masuala ya amani, migogoro, na usalama yalibainishwa pia katika utafiti huu. Wakati kukiwa na mitazamo inayokinzana kuhusu nafasi ya madereva  wa bodaboda katika migogoro kati ya serikali na maafisa wa usalama (ambao wanawaona madereva wa  bodaboda kuwa wahalifu wa migogoro) na madereva wa bodaboda (wanaojiona wahanga na waathirika wa migogoro na matumizi ya nguvu kupita kiasi dhidi ya polisi), Utafiti huu umeibua mtazamo wa tatu unaowatambua madereva wa bodaboda kama mawakala na wadau muhimu katika kudumisha amani na usalama. Mbali na kusafirisha abiria, madereva wa bodaboda wanashiriki katika ulinzi jirani katika kudumisha amani na usalama na hushirikiana na polisi kwa kuwapa taarifa za matukio ya kiuhalifu.Vyama vya mederava wa bodaboda vimewapa vijana nafasi ya kujadili na kudumisha amani na kuziba pengo kati ya madereva wa bodaboda na polisi na serikali.

**Kwa upande wao, wanajamii na vijana walielezea kuwa ngoma na nyimbo za asili ni nyanja mathubuti na zinazopendelewa zaidi katika kuleta mshikamano ndani ya jamii.**

Dini inaweza kuwa nafasi nyingine mudhubuti katika kuhimiza ushiriki wa vijana. Ingawa mara nyingi vijana hawajihusishi moja kwa moja na masuala ya kidini, uzoefu umeonyesha kuwa jamii na vijana wana mwelekeo wa kuwaamini viongozi wa dini kuliko serikali na polisi. Hivyo viongozi wa dini na kamati mbalimbali za kidini zimeonyesha umuhimu katika kukuza ushiriki wa vijana na kuziba pengo kati ya serikali, polisi na vijana.

Mwishowe, maeneo ya mikusanyiko isiyo rasmi yanayojulikana kama vijiwe ambapo wanawake na wanaume hufanya mikusanyiko tofauti nyakati za  jioni yalitambuliwa kama maeneo muhimu ya kubadilishana mawazo, taariifa na mambo mengine ya msingi yahusuyo jamii. Hususani, mikusanyiko ya wanawake imekuwa jukwaa muhimu ambamo huchangishana fedha zinazohitajika kugharamia biashara wanazomiliki na na wameunda vikundi vya uwezeshaji wanawake kiuchumi (VICOBA) vinavyo toa mikopo midogo midogo kwa wanawake. Zaidi ya hayo, utafiti uligundua matukio ambapo taarifa zilizotolewa kupitia mikusanyiko hii isiyo rasmi zilisaidia jamii na serikali kugundua na kukabiliana na vitisho vya usalama na matatizo mengine kama vile ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa watoto.



©PHOTOVOICE WEWORLD

## 2 Mitazamo ya jamii juu ya vijana na jukumu lao katika masuala ya amani na usalama

Jamii ina mitazamo mchanganyiko juu ya vijana kuhusiana na jukumu na wajibu wao katika masuala ya amani, migogoro, na usalama.Wazee, ambao wanachukuliwa kuwa walinzi wa utamaduni na wana mamlaka juu ya masuala ya kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi ndani ya jamii, wana maoni na mitazamo hasi juu ya vijana. Mara nyingi waliwaelezea vijana kuwa ni kundi ambalo limepoteza maadili na mwelekeo. Kulingana na wazee, vijana hawasikii na hawashiriki katika mikutano rasmi ya vijiji. Kwa upande mwingine, wazee hawakutoa maoni yao kuhusiana na vijana wa kike, labda ni kutokana na mtazamo wa majukumu ya kijinsia ambapo wanawake huonekana kuwa hawana umuhimu sana kwenye masuala yanayohusu amani, migogoro, na usalama.

Maafisa wa serikali na Polisi waliwaona vijana kwa njia mbili tofauti. Kwa upande mmoja, walitambua mchango chanya wa vijana walioshiriki katika mfumo wa ulinzi shirikishi katika kusaidia kupunguza migogoro na vitisho vya usalama. Hata hivyo, Ikumbukwe kwamba mitazamo hii imejikita katika mfumo wa ulinzi shirikishi, ambao ni jukwaa mahususi na linalokubaliwa na serikali na polisi. Kwa upande mwingine, Polisi na maofisa wa serikali waliunga mkono maoni hasi ya wazee juu ya vijana. Kwa mujibu wa polisi na maafisa wa serikali, vijana wanadaiwa kuhusika katika utoaji wa msaada kwa watuhumiwa wa ghasia za itikadi kali kwenye mpaka wa Mtwara na kaskazini mwa Msumbiji. huko Tanga, maafisa wa serikali na Polisi waliwashutumu vijana kwa kuwezesha shughuli haramu, haswa, kuwavusha mpaka wahamiaji haramu na usafirishaji wa mirungi (miraa).

> **Kulingana na wazee, vijana wa kiume sio wa sikivu na huwa hawashiriki katika mikutano rasmi ya kijiji.**



## 3 Sababu zinazowakwamisha vijana kuwa na ushiriki chanya katika masuala muhimu ndani ya jamii zao

Vijana kubaguliwa na kutengwa, matatizo ya kiuchumi na uwepo wa dini zenye itikadi na misimamo mikali zimebanishwa kuwa ndio sababu kuu zinazowakwamisha vijana kuwa na ushiriki chanya masuala muhimu ya jamii.

Vijana wa kiume walielezea wasiwasi wao kuhusu kutengwa na kubaguliwa kwa maslahi ya vijana (hasa ya kiuchumi) na sauti zao katika jamii. Ingawa vijana wa kike nao wametengwa kiuchumi sawa na vijana wa kiume, hawakuibua wasiwasi kama hizo. Hii inachangiwa na ukweli kwamba mambo yanayohusu masuala ya kiuchumi ndani ya jamii yanatawaliwa na wanaume. Vijana wana mtazamo kuwa sauti na maoni yao  hayachukuliwi kwa uzito kwa sababu vyombo rasmi vya maamuzi katika jamii na serikali vinadhibitiwa na kutawaliwa na wazee. Hasusani, vijana walilalamikia kuhusu mila na desturi za kitamaduni ambazo zinawapa wazee mamlaka ya kudhibiti ardhi. Kwa upande wao, wazee wanadai wanathibiti ardhi hadi vijana watakapokuwa wakubwa kwa sababu wanahofia kuwa vijana hawataweza kuisimamia vizuri ardhi na pia wanaweza kuiuza.

Pili, kwa mtazamo wa vijana wengi hasa madereva wa bodaboda, ukatili kutoka katika  jeshi Polisi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vinavyoshika doria mipakani bado ni changamoto inayowakwamisha vijana kutekeleza majukumu na wajibu chanya ndani ya jamii.  Ukatili wa polisi umezua hali ya kutoaminiana kati ya vijana na polisi, kiasi kwamba vijana hawaoni umuhimu wa kushirikiana na Polisi katika kutafuta suluhu ya changamoto za  kiusalama. .

Mwishowe, uwepo wa mafundisho ya itikadi kali za kidini husababisha migawanyiko katika jamii na kukwamisha ushiriki wa vijana katika masuala ya kijamii. Hii ni kwa sababu tafsiri ya kihafidhina ya Uislamu inapinga mila na desturi za kitamaduni, kama vile ngoma, muziki, matambiko na sherehe za kidini na kimila. Huko Tandahimba na Newala na baadhi ya maeneo ya vijiji vya Mtwara, kutokuelewana kati ya waislamu wa Salafi na wanajamii wengine imeonekana dhahiri.

**Kulingana na mtazamo wa vijana, sauti za vijana hazizingatiwi kwa sababu vyombo rasmi vya maamuzi ndani ya jamii na serikalini vimedhibitiwa na wazee.**

## 4 Udhihirishaji wa maadili, mila na desturi za utamaduni wa Waswahili

Utafiti ulionyesha ni kwa namna gani maadili kama vile ukarimu na mshikamano wa kikabila, mila na desturi za kidini na kitamaduni kama vile, sherehe, muziki na ngoma za asali, na matambiko yanavyochangia katika kuleta mshikamano katika jamii za Tanga na Mtwara.

Ukarimu ni tunu inayoonyesha tamaduni na desturi inayodumishwa na jamii za Tanga na Mtwara ambayo inajidhihirisha kwa njia tofauti. Kwanza, kwa kushiriki chakula na wageni ambapo chakula huandaliwa nje ya nyumba ili watu wote wakutane wakati wa kula. Jamii za Waswahili wa Pwani huamini kuwa wageni ni lazima waburudishwe ili wasirudi makwao wakiwa na mtazamo au picha mbaya ya wanyeji wao. Kitendo cha kula chaula pamoja hukuza mshikamano wa familia na jamii na hutumika kama nafasi kwa wazee kuzungumza na vijana kuhusu masuala yanayohusu amani, migogoro, na usalama. Pili, ukarimu hujidhihirisha kwa kusaidiana wakati wa mazishi na harusi. Hususani, wanajamii huchangiana rasilimali za kifedha na zisizo za kifedha kwa ajili ya kufanya mazishi, harusi na sherehe za kitamaduni. Maandalizi na ushiriki katika harusi huhusisha watu kutoka ndani na nje ya jamii husika.

Tunu nyingine ambayo imejikita sana katika utamaduni hasa katika makabila makubwa kama vile Wadigo huko Tanga (na Kwale) na Wamakonde huko Mtwara (na Kaskazini mwa Msumbiji) ni imani kwamba wote ni ndugu. Hili linakuzwa zaidi na dini ya Kiislamu inayoendeleza mafundisho kwamba Waislamu wote ni ndugu. Imani hii inabeba hisia ya mshikamano na wajibu wa pamoja kwa wanajamii wote katika kabila hilo kuwa watunzaji na walinzi wa wanajamii wengine. Ni jambo la kawaida kuona watu wa kabila moja wakivuka mipaka ya nchi na kujiunga na sherehe za wanajamii wa upande mwingine.


**Ngoma na nyimbo za asili husambaza ujumbe wa amani na pia hutumika kama jukwaa la usuluhishi ndani ya jamii.**

Hata hivyo, ikumbukwe kuwa serikali na vyombo vya ulinzi na usalama vilitoa angalizo kuwa mila na desturi za kulindana ni chanzo cha matatizo ya kiusalama kwani imewaruhusu watuhumiwa wa ghasia za itikadi kali na wasafirishaji magendo kutorokea mipakani na kupewa ulinzi kutoka kwa wanajamii kwa upande mwingine.

Sherehe za kidini na matambiko ya kimila huunganisha wanajamii wanaoishi ndani na nje ya Tanga na Mtwara . Wanajamii hurudi makwao ili kuungana na familia na jamii zao katika kusherehekea Maulid na kufanya matambiko ya kimila. Sherehe na mikusanyiko huimarisha uhusiano baina ya wanajamii na hutoa nafasi ya kubadilishana mawazo kati ya vijana na wazee na wanajamii wengine na hutumika katika kufanya suluhu ya migogoro ndani ya familia na jamii. Ngoma za kimila na muziki hubeba na kusambaza jumbe za amani na pia hutumiwa kama njia ya upatanishi katika jamii. Hasa, nyimbo za kawaida, kama vile 'baba na mama', katika kabila la Wamakonde huhimiza wanajamii kuepuka kulipiza kisasi. Pia ngoma kama vile Mzobe huko Mtwara na Mduara huko Tanga hutumika kuashiria amani. Wakati wa maonyesho ya ngoma hizi, wanajamii hukutana na kugusana, ikiwa ni ishara ya amani na kumaliza tofauti zozote baina yao. Methali za kitamaduni ambazo zinaweza kudumisha amani au uchochezi pia zinajumuishwa kwenye mavazi ya kitamaduni kama vile kanga zinazovaliwa na wanawake.

# Uchunguzi kifani kutoka Kenya

Uchunguzi huu kifani unachunguza nafasi ya vijana katika kudumisha amani na mchango wa tamaduni za Waswahili katika kuhamasisha amani katika kaunti ya Kwale (kwenye tarafa za Lunga Lunga, Msambweni na Matuga) nchini Kenya.



## 1 Ni kwa namna gani vijana wanashiriki katika mijadala ya kijamii inayohusiana na masuala ya amani, migogoro, na usalama

Utafiti huu umebaini majukwaa kadhaa yatakayowawezesha vijana kushiriki katika mijadala ya kijamii kuhusu amani, migogoro, na usalama, yaani majukwaa ya kiraia, sherehe za kijamii, mifumo rasmi ya ulinzi na usalama katika jamii (kamati za amani na nyumba Kumi), vikundi vya boda boda, na taasisi za kidini.

AZAKI (CSOs), asasi za kijamii (CBOs), na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yaliyopo Kwale nchini Kenya yamekuwa ni majukwaa muhimu ya kuwafikia na kuwashirikisha vijana katika masuala ya amani, migogoro, na usalama. Yote haya yamefanyika kupitia mikakati ya kujenga uwezo, mshikamano, na kuaminiana, kupitia upatanishi na utatuzi wa migogoro wa moja kwa moja, kuongeza uwelewa pamoja na uhamasishaji ndani ya jamii, na kwa kuwawezesha makundi yaliyotengwa na kukandamizwa ndani ya jamii kama vile wanawake, vijana, na masikini. Asasi hizi ni sehemu ya mtandao mpana wa vijana ambao hujumuika katika shughuli za kijamii na kushiriki kwenye mabaraza[6] ,ya maamuzi ndani ya jamii, pamoja programu za kujenga uwelewa kwa jamii, na mikakati mengine inayohusiana na masuala ya usalama katika jamii. Jumuiya za vijana ndani miundo hii ya taasisi za kijamii huwa ni majukwaa muhimu kwa ajili ya usambazaji taarifa zinazohusu udumishaji wa amani na mshikamano ndani ya jamii, ili kupaza sauti za vijana wa kike na kiume. Muhimu zaidi, wanawake wamekuwa vinara katika vikundi vya upatu na VICOBA, AZAKI, na asasi za kijamii.

Hata hivyo, vijana na wanawake wanaoshirikishwa katika masuala haya ya kijamii ni wachache mnoo na muda mwengine hualikwa katika majukwaa ya majadiliano ya masuala ya amani, migogoro, na usalama kama 'geresha' tu ili kuonesha ushirikishwaji wa makundi mbali mbali badala ya kuthamini michango chanya kutoka kwa makundi haya kwenye mijadala husika.

Utafiti huu umejikita katika mifumo miwili rasmi ya usalama ya kiserikali. Nayo ni kamati za amani na mfumo wa nyumba kumi (nyumba kumi hutumika zaidi katika tarafa ya Lunga Lunga). Kamati za amani hutoa mafunzo kwa vijana kuhusu utatuzi wa migogoro, udumishaji wa amani, na upatanishi wa migogoro. Kwa siku za nyuma, mafunzo haya yamefanikisha kujenga uhusiano wa karibu baina ya vijana kutoka makundi mbali mbali na yamehamasisha maelewano na kuheshimiana miongoni mwa vijana na yamewawezesha vijana kukuza ujuzi unaohitajika ili kutatua migogoro kwa amani na pia kuhamasisha amani na mshikamano ndani ya jamii zao, hususani katika kipindi ambacho shughuli za usajli wa vijana katika makundi yenye msimamo mkali zilikuwa zimeshika kasi. Hata hivyo, utafiti huu umebaini kuwa uwiano wa ushiriki wa makundi mbali mbali katika kamati za amani umeegemea zaidi kwa wazee, kama watendaji wa serikali au maafisa usalama.

Msingi wa mfumo wa Nyumba Kumi umejikita zaidi kuimarisha amani, hata hivyo, kwa baadhi ya maeneo mfumo huu umekuwa jukwaa muhimu ambapo watu wa rika mbali mbali hupaza sauti zao kuhusu changamoto zao, kutatua masuala ya kijamii, na pia kuanzisha shughuli za biashara. Hata hivyo, ushiriki wa vijana katika mfumo wa nyumba kumi bado ni duni.

6. Baraza ni mkutano wa maamuzi - ni mkutano wa wanajamii, mara nyingi huwa ni mkutano wa hadhara, na huitishwa kujadili masuala ya ustawi wa jamii.

Miongoni mwa majukwaa yasiyo rasmi, sherehe za kijamii mathlan harusi na mazishi zimebainika kuwa ni matukio muhimu ambayo yamekita mizizi katika tamaduni za Waswahili ambapo huwa ni kiunganishi muhimu ndani ya jamii, kwani huwa ni sehemu muhimu ya kujenga mshikamano wa jamii, majadiliano, na kukuza ushirikiano ndani ya jamii. Mikusanyiko kama hii ya kijamii huvutia hadhara kubwa ya watu, na mara nyingi huhusisha watu mbali mbali ikiwa ni pamoja na vijana wa kike na kiume ambao hawajihusishi sana na mifumo rasmi kama vile AZAKI na majukwaa rasmi ya kiusalama katika jamii.[7] Zaidi, vijana (hasa vijana wa kiume) ambao mara nyingi huwa hawajihusishi sana na masuala ya kijamii hujumuika katika maskani kwa ajili ya kupiga soga na kubadilishana mawazo. Maskani hizi huwa ni majukwaa muhimu ya kusambaza matangazo na taarifa mbali mbali kwa umma. Baadhi ya AZAKI mara kwa mara hutumia sherehe hizi za kijamii kuhamasisha amani na mshikamano ndani ya jamii.

Waendesha Boda boda pamoja na jamuiya zao (kama SACCO) zimekuwa ni majukwaa muhimu yaliyopo ambayo yamekita mizizi ndani ya jamii hususani husaidia kufanikisha ushiriki wa vijana wa kiume katika masuala ya amani, migogoro, na usalama katika ngazi za chini. Ijapokuwa sekta ya Boda boda hutazamwa na wengi kama chanzo cha uhalifu, utafiti huu umebaini vikundi vya boda boda hapo awali vilishiriki katika kutatua migogoro ndani ya sekta hiyo na kubaini wahalifu ambao hujifanya kutoa huduma kwenye sekta ya boda boda. Wakati mwengine sekta ya boda boda hushiriki kwenye miradi ya kijamii na huwa na umuhimu zaidi kipindi cha uchaguzi ambapo jumuiya zao hukutana na wanasiasa ili kuwasilisha changamoto na mapendekezo yao. Hata hivyo, bado boda boda wana uhusiano tata na watunga sera, wadau wa usalama, na jamii.

> **Asasi za vijana ndani ya jamii huwa ni nyanja muhimu katika usambazaji wa taarifa kuhusu udumishaji wa amani na mshikamano, na pia katika kupaza sauti za vijana wa kiume na wa kike.**

Mwisho kabisa, taasisi za dini zimekuwa na historia ya upatanishi na utatuzi wa migogoro ndani ya jamii. Taasisi hizi zinauwelewa wa kina kuhusu utamaduni wa jamii husika, maadili yao, na mico iliyopo ambapo huwapa uwezo mkubwa wa kuimarisha na kudumisha amani katika jamii husika. Jamii zinawaheshimu sana viongozi wa dini and huwa na utayari wa kusikiliza mahubiri yao kuhusu amani na maridhiano. Hata hivyo, viongozi wa dini ni wazee mnoo, haliyakuwa vijana, hasa wanawake, wana ushiriki duni sana kwenye nyanja za kidini.

Kwa ujumla, utafiti umebaini utofauti mkubwa kwenye kiwango cha ushiriki wa vijana katika masuala ya amani na usalama kulingana na vitongoji vyao na jinsia zao. Vijana ambao wanaishi tarafa za mijini mathalan Msambweni na Matuga wanashiriki zaidi kwenye majukwaa ya amani na usalama kuliko wale ambao wanaoishi tarafa za vijijini kama vile Lunga Lunga. Hata ndani ya tarafa utofauti kati ya mjini na pembezoni mwa mji hudhihirika. Kwa mfano, maeneo Matuga mjini, watu wengi wamekumbatia dhana ya jumuiya za vijana na mchango wao ndani ya jamii, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha amani. Hata hivyo, hii imebakia kuwa ni changamoto kubwa pembezoni mwa mji wa Matuga. Pili, vijana wa kiume wana uwakilishi mkubwa zaidi katika masuala ya amani na usalama katika jamii kuliko vijana wa kike. Uwakilishi duni wa vijana wa kike una akisi jamii ya mfumo dume iliyopo kaunti ya Kwale.

7. Kwa miaka ya hivi karibuni, harusi na sherehe nyengine za kijamii zimekuwa zikilengwa na mashumbulizi na uvamizi kutoka kwa magenge ya vijana ambayo huendesha shughuli zao kaunti ya Kwale, hivyo kupunguza thamani ya sherehe hizi kama majukwaa muhimu ya kudumisha mshikamano na amani katika jamii.

## 2 Mitazamo ya jamii juu ya vijana na jukumu lao katika masuala ya amani na usalama

Kwa ujumla, vijana wa kike na kiume katika kaunti ya Kwale hawatazamwi kama wana mchango chanya katika majadiliano kuhusu amani na usalama bali hutazamwa kama wavunjifu wa amani na usalama. Wazee ambao wapo kwenye nafasi za maamuzi mathalan kwenye nafasi za utendaji serikali kuu na serikali ya kaunti huwalaumu vijana kwa kuongezeka kwa matukio ya wizi, mashambulizi dhidi ya wazee, matumizi ya dawa za kulevya, na kwa ujumla uvunjifu wa sheria nchini. Sababu ambazo hutolewa kuhusu matukio haya huwa ni ukosefu wa ajira, upweke, matumizi ya dawa za kulevya, mmomonyoko wa maadili na mila na desturi kongwe za Waswahili, pamoja na uchu wa kupata fedha haraka, na ukosefu wa malezi bora.

Wadau mbali mbali hutambua uwezo wa vijana kuchangia katika masuala ya amani, hata hivyo, wakongwe wengi huhisi kuwa vijana ni lazima waongozwe na kupatiwa mafunzo kuhusu mila na desturi za tamaduni za Waswahili. Wakongwe huhoji uwezo wa vijana kushika hatamu za uongozi. Msemo wa Kidigo “ngoma ya anache taichesa” (ngoma ya mtoto haichezwi usiku) hutumika mara kwa mara na wakongwe kuashiria kuwa hatua zozote zinazochukuliwa na vijana au ‘watoto’ huwa hazidumu, na kwahiyo, wakongwe ni lazima wawe mstari wa mbele katika kuwaongoza vijana. Vijana wa kike na wasichana hukandamizwa mara dufu katika masuala yanayohusu amani na usalama katika jamii kwa sababu ya kukita mizizi kwa mfumo dume ndani ya jamii.

## 3 Sababu zinazowakwamisha vijana kuwa na mchango chanya katika masuala muhimu ndani ya jamii zao

Kwa vijana ambao hujihusisha zaidi na masuala ya kijamii changamoto kadhaa hukwamisha mchango wao katika masuala yanayohusu amani na usalama. Hii ikiwa ni pamoja na uhaba wa rasilimali fedha, utitiri wa asasi za kijamii (CBOs), AZAKI, na mashirika ya yasiyo ya kiserikali (NGOs) katika vitongoji vingi huku wakishindania rasilimali chache, ukosefu wa elimu kuhusu masuala ya fedha na ujuzi mdogo kuhusu usimamizi wa miradi, uwezeshaji mdogo kutoka kwa wanasiasa wa serikali kuu na serikali ya kaunti, wasi wasi na ukosefu wa uwezeshaji wa wanajamii, kupungua hali ya kuaminiana ndani na kati ya AZAKI, uwakilishi duni wa vijana wa kike katika asasi za kijamii, na ukosefu wa malengo mahususi ya kitaasisi.

Ukiachilia mbali changamoto hizi, vijana ambao hujihusisha zaidi na masuala ya kijamii huleta uzoefu muhimu na mtazamo wa kina katika ushirikishwaji wa jamii katika masuala yenye tija kwa jamii zao. AZAKI, CBOs, na NGOs zimejenga uhusiano mzuri na serikali ya kaunti ya Kwale, hatua hii imetengeneza mazingira rafiki ya utatuzi wa migogoro, usalama, na harakati za kudumisha amani katika kaunti.

## 4 Udhihirishaji wa maadili, mila na desturi za utamaduni wa Waswahili

Utafiti huu umebainisha misingi ya maadili na desturi za kitamaduni na kidini ambazo huhamasisha amani na mshikamano ndani ya jamii za Kwale. Baadhi ya mila na desturi kwa sehemu kubwa ni za kale na kwa sasa hazitumiki lakini zinaweza kuwa nguzo muhimu ya kuhamasisha amani katika jamii husika.

Utafiti huu umebaini kuwa misingi ya maadili ya tamaduni za Waswahili kaunti ya Kwale na ile ya dini ya Kiislamu inawiana. Tamaduni zote mbili (za Waswhili na ya dini ya Kiislamu) zinahimiza kuishi pamoja na kuhamasisha ujamaa. Misingi hii ya maadili hudhihirika kipindi cha mfungo wa Ramadhani na sikukuu ya Iddi ul-Hajj, ambapo Waislamu hujumuika kula pamoja na pia kuwasaidia wasiyojiweza. Desturi kama hii pia ipo kwenye tamaduni za Waswhili, na hutambulika kama Aro, ambapo ndugu na jamaa hupika chakula pamoja na hula pamoja ili kuhakikisha hamna anaekosa chakula.

Tamaduni za Waswahili huhimiza vikao vya mara kwa mara vya familia ambapo ndugu na jamaa hujumuika pamoja, hushikamana, na huimarisha mahusiano. Desturi hii huhamasisha amani na utatuzi wa migogoro, kwani wanafamilia huwa na fursa ya kupatia ufumbuzi masuala ambayo yanaathiri mshikamano wa familia. Mikusanyiko ya kijamii kama harusi huleta pamoja jamii na hupambwa na ngoma na nyimbo ambazo huimarisha ushirikiano miongoni mwa wanafamilia.

Mila na desturi ambazo zimekita mizizi katika kaunti ya Kwale na kihistoria zimetumika kuhamasisha amani na mshikamano ndani ya jamii ni pamoja na ‘mweria’ (pia wiri, ambayo hujumuisha ushirika na mashirikiano miongoni mwa wanajamii). Hii desturi humaanisha kuwa wanajamii huja pamoja ili kusaidiana katika ujenzi wa nyumba, kulima, kuvuna mazao, n.k. Desturi hii hukuza ushirikiano, kuishi pamoja, na huimarisha amani miongoni mwa wanajamii.

Hadi hivi leo, maeneo ya asili ya matambiko msituni ambayo hujulikana kama Kaya bado yanabeba umuhimu mkubwa wa kiimani na kimila ndani ya jamii za Kwale. Ijapokuwa wakati mwengine vijana huhusishwa katika miradi ya uhifadhi wa misitu ya Kaya, kulinda ardhi za Kaya kutokana na uvamizi, na kukabiliana athari za mabadiliko ya tabia ya nchi katika maeneo haya matakatifu, Kaya zimebakia kuwa ni nyanja za kitamaduni ambazo zimetawaliwa zaidi na wazee.

**Tamaduni za Waswahili kaunti ya Kwale na ile ya dini ya Kiislamu inawiana. Tamaduni hizi huhimiza kuishi pamoja na kuhamasisha ujamaa baina ya wanajamii.**

# Hitimisho na Mapendekezo

Utafiti huu umebaini kuwa mchango wa vijana katika masuala ya amani na usalama hukwamishwa na sababu mbali mbali mathalan ukosefu wa rasilimali za kiuchumi, hali ya kutoaminiana baina ya vijana na wazee, hasa wazee ambao ni wadau wa usalama, na ukandamizwaji wa vijana katika nafasi za maamuzi. Kwa upekee, uwepo mitazamo sugu kuhusu vijana kuwa na uwezo mdogo wa kuhamasisha amani na usalama umewakwamisha kuwa na mchango chanya katika masuala ya amani na usalama.

Vijana hushiriki katika mijadala ya jamii kuhusu amani, migogoro, na usalama kupitia majukwaa mbali mbali. Hata hivyo, majukwaa haya mengi yamejikita katika masuala ya usalama, na vile vile huwatenga wanawake kwani yamedhibitiwa mnoo na wakongwe ndani ya jamii. Zaidi, majukwaa yasiyo rasmi na yale ambayo yametaliwa na vijana mara kwa mara hayathaminiwi na aghlabu hutumika na wadau (kama vile NGOs, INGOs, na mamlaka za kitaifa na mitaa) ambao hulenga kuongeza mchango wa vijana katika udumishaji wa amani na utulivu. Mila na desturi ni vyanzo muhimu vya mshikamano katika jamii, huku zikitoa fursa ya kuimarisha ushirikishwaji hasa wa vijana wa kiume na wa kike. Wadau wakuu wanapaswa kuupa umuhimu uwezo wa vijana na uwezo uliyopo wa misingi ya tamaduni za Waswahili na desturi zao katika kuchangia amani na usalama.


©PHOTOVOICE WEWORLD

## Kuwezesha Majukwaa ya kitamaduni ambayo aghlabu hutumika kwa ajili masuala ya amani na kuongeza matumizi ya mila na desturi za Waswahili ambazo huhamasisha amani katika jamii

**Mamlaka za kidola wakiwemo wadau wa usalama, AZAKI, na jumuiya pana za wadumishaji amani ni lazima watambue mchango wa kipekee wa mila na desturi kama vile sherehe, ngoma, na nyimbo katika kuimarisha mshikamano na amani, na kuanzisha mikakati ya kutumia zaidi nyanja hizo. Kwa mfano,**

— Kujenga ubia na ushirikiano baina ya wadau wakuu kama vile AZAKI, taasisi za kitamaduni (za kiserikali na zisizo za kiserikali), viongozi wa dini, maafisa utamaduni katika wilaya, na viongozi kwenye jamii ili kuhamasisha matumizi ya majukwaa ya kitamaduni na desturi ambazo hujumuisha vijana.

— Kufanya kazi na wandaaji wa sherehe (kama vile maulidi, harusi, n,k.) na wacheza ngoma na nyimbo za asili ili kuhamasisha misingi chanya ya tamaduni za Waswahili kama vile kujaliana, umoja, na ushirikiano miongoni mwa vijana na jamii.

— Walimu, shule, na AZAKI zitumie mila na desturi, misingi ya maadili, ngoma na nyimbo ambazo zinahamasisha misingi ya amani katika kushirikiana na watoto na vijana.

— Kutengeneza nafasi kwa maafisa wa serikali na usalama kutambua na kushiriki sherehe za kitamaduni ambazo huhamasisha na kutumbuiza mila na desturi ambazo huhamasisha amani katika jamii. Hili linaweza kujumuisha kuandaa siku ya utamaduni mashuleni ambapo wanafunzi wanaweza kuandaa kazi za sanaa na kubadilishana kazi hizo ambazo zinainisha mchango wa utamaduni katika kuhamasisha amani.

— Wazee wanapaswa kuruhusu na kuhamasisha vijana kushika hatamu za uongozi katika sherehe na nyanja zengine za kitamaduni. Kwa mfano, nchini Kenya, tunaweza kuchunguza zaidi ushirikiano baina ya wazee na vijana katika kuhifadhi maeneo ya kitamaduni ya Kaya.

— Wanahabari na vyombo vya habari hupaswa kuandika na kusambaza maudhui ambayo yanaonesha mchango wa mila na desturi zinazohamasisha amani yakilenga kuonesha mchango wao katika kuimarisha mshikamano ndani ya jamii.

## Kubadili mitazamo ya vijana na kujenga mahusiano mazuri baina vijana na wazee ndani ya jamii pamoja na wadau wa usalama serikalini

**Ili kutengeneza mazingira ya vijana kuchangia na kushawishi zaidi maamuzi yanayohusu masuala ya amani na usalama kwenye jamii zao, jitihada zinahitajika kubadili namna ambavyo vijana wanatizamwa katika jamii na viongozi wake (wale wenye nyadhifa rasmi na zisizo rasmi) pamoja na kubadili mahusiano baina vijana na wazee ndani jamii pamoja na wadau wa usalama serikalini. Kwa mfano:**

- AZAKI, jumuiya pana za wahamasishaji amani, viongozi katika jamii, na maafisa wa serikali wanapaswa kuhamasisha na kufanikisha mjadala wa rika mbali mbali ili kujenga uwelewa wa pamoja baina ya wazee na vijana wa kiume na wa kike, kwa kujikita katika mjadala kuhusu mila na desturi na namna gani desturi hizi zinaweza kutumika kuhamasisha amani kama sehemu ya kuanzia.

- Mikakati ya kuunganisha baina wazee na vijana na kati ya wadau wa usalama serikalini na vijana inapaswa kuchunguza mchango wa viongozi wa dini katika kuhuisha na kuimarisha mahusiano.

- Mbinu mbali mbali za kuboresha mahusiano baina ya vijana wa kiume na wa kike na wazee na wadau wa usalama serikalini zinapaswa kuchunguzwa, mbinu hizo ni kama vile michezo, nyimbo, na maigizo.

- Shule zinapaswa kutengeneza fursa kwa wazee kuchangamana na wanafunzi, kwa mfano katika masuala yanayohusiana na mila na desturi kuptia mazungumzo ya pande mbili badala ya mhadhara wa upande mmoja kwa wanafunzi

- Vyombo vya habari na wanahabari wanapaswa kuwajengea vijana wa kiume na wa kike taswira njema kwa kuonesha mchango wao katika masuala ya amani katika jamii kupitia nyanja mbali mbali, ikiwemo majukwaa ya kitamaduni na mikusanyiko ya ‘kila siku’ kama vile vijiwe, maskani, VICOBA/chama (vikundi vya akiba na mikopo), boda boda, sherehe, n.k.

## Kutanua wigo na ubora wa ushirkishwaji wa vijana wa kike na kiume katika nyanja rasmi za usalama katika jamii

**Kuimarisha mchango wa majukwaa rasmi yaliyopo katika jamii ili kudumisha usalama na kuimarisha amani, lakini jitihada zinahitajika kuyasogeza majukwaa haya karibu zaidi na jamii na kugatua mfumo wake wa maamuzi ili kuwapa jukumu kubwa vijana katika kushawishi maamuzi ndani majukwaa haya. Kwa mfano:**

— Kufanya mijadala ya pamoja na jumuishi baina ya vijana wa kike na wa kiume na maafisa serikalini na viongozi katika jamii kuhusu kutanua wigo wa ushiriki na ushawishi wa vijana katika majukwaa yaliyopo ambayo yamehodhiwa na wazee kama vile mifumo rasmi ya usalama na taasisi za kidini.



— Kufanya mapitio ya miundo ya usimamizi wa usalama kama vile ulinzi shirikishi, nyumba kumi, na kamati za usalama pamoja na kuwashirikisha jamii na vijana wa kike na wa kiume katika mijadala inayohusu namna gani miundo hii ya usalama iongozwe na jamii na kwa namna gani usimamizi wake uanzie ngazi za chini huku ikihusisha usimamizi wa vijana wa kike na wa kiume katika uendeshaji wake.

— Wakati wa uchaguzi wa vijana kushiriki kwenye vyombo rasmi vya maamuzi katika jamii, kipaumbele kiwe ni kuwafikia vijana na wanawake ambao wamekandamizwa na kutengwa ili kuwahamasisha kushiriki kwenye kuwania nafasi za uwakilishi kwenye vyombo vya maamuzi katika jamii.

**Kutanua wigo wa ushiriki na ushawishi wa vijana katika majukwaa yaliyopo ambayo yamehodhiwa na wazee.**

## Kulenga kuwashirikisha vijana wa kike na wa kiume waliokandamizwa ambao mara nyingi hutengwa kwenye mijadala kuhusu amani na usalama katika jamii

**Ni lazima mikakati yoyote ambayo imelenga kuhamasisha ushiriki na ushawishi wa vijana katika maamuzi yanayohusu masuala amani na usalama yajikite dhahiri shahiri katika kuwashirikisha vijana ambao bado hawapo kwenye vyombo rasmi vya maamuzi; na hususani kuinua mchango wa vijana wa kike katika masuala ya amani na usalama. Kwa mfano:**

— Kufanya utafiti wa ziada ambao utaangazia jukumu na mchango wa vijana wa kike katika masuala ya amani na usalama na pia kutafiti mila na desturi kwa mrengo wa kijinsia, nia ni kubaini mila na desturi chanya ambazo zinaweza kuhamasisha zaidi uwezeshaji wa wanawake.

— Kuwahusisha vijana wa kike na kiume katika masuala ya amani na usalama hasa kwenye maeneo ambayo tayari wana ushiriki mkubwa kama vile mashuleni, vikundi vya boda boda, asasi za kijamii (VICOBA na chama kwa wanawake), mikusanyiko isiyo rasmi (kama vile vijiwe na maskani), na sherehe kama vile harusi na maulidi.

— Maafisa serikalini, viongozi ndani ya jamii, mashirika ya kimataifa, na wahisani wanapaswa kusaidia jumuiya za vijana ili kuweza kuwafikia na kuwahamasisha vijana ambao wamejitenga na jamii kupitia ushawishi wa makundi rika ili nao kuwahusisha moja kwa moja katika masuala ya amani na usalama (kupitia majadiliano, nafasi za maamuzi n.k.) pamoja na kuwashirkisha kupitia njia isiyo ya moja kwa moja (kupitia shughuli za sanaa, ngoma, na nyimbo, n.k.).

— Shule na walimu wanapaswa wa kuwahusisha vijana wa kike na wa kiume katika mazungumzo na shughuli zinazohusu utamaduni na amani kwa usawa nia ikiwa ni kutokomeza ubaguzi wa kijinsia.

— Wanahabari na vyombo vya habari vinapaswa kubainisha mchango chanya wa vijana wa kike na wa kiume waliyokandamizwa na kutengwa katika masuala yanayohusu amani ndani ya jamii hasa kupitia maudhui wanayoandaa nia ikiwa ni kutokomeza ubaguzi dhidi ya makundi mbali mbali, kama vile vijana wa kike, na waendesha boda boda, n.k.

**Kuwahusisha vijana wa kike na kiume kwenye majukwaa ambayo tayari wana ushiriki mkubwa kama vile mashuleni, vikundi vya boda boda, na asasi za kijamii.**

WeWorld Member of ChildFund Alliance
Peaceful Change initiative
HORN International Institute for Strategic Studies
University of Dar es Salaam
Co-funded by the European Union